

# Uhalifu biashara ya utalii Zanzibar ukomeshwe

Zanzibar inavyoonekana ufukweni mwa Bahari ya Hindi. Picha na Maktaba.

## HABARI ZAIDI

**-Mfumo wa kisheria unahitajika ili kuhakikisha ulinzi na usalama wa watalii wanaotembelea Zanzibar.**

**-Kanuni na mfumo wa kisheria unapaswa kupitiwa upya na mapendekezo yanapaswa kutolewa ili kuweka misingi imara ya kisheria kwa ajili ya ulinzi na usalama wa watalii.**

**- Kuangalia fursa zilizopo ambazo zitatumiwa kuwaleta watalii wanaotaka kutumia vyema fedha zao kama watalii na wawekezaji.**

**Lengo la kuwapo kwa kikosi cha ulinzi ni kuwadhibiti wahalifu wasiwabugudhi watalii Zanzibar.**

Veneranda Sumila, Mwananchi

Shirikisho la Wawekezaji katika Sekta ya Utalii Zanzibar (Zati) linafanya kila juhudi kuhakikisha usalama kwa watalii wanaotembelea visiwa vya Zanzibar.

Kutokana na juhudi hizo Serikali kwa kushirikiana na Zati wanakusudia kuimarisha ulinzi na usalama kwa watalii ili kulinda mitaji na mapato ya wawekezaji kwa kuwa ulinzi imara utachochea watalii wengi viziwani Zanzibar na kuongeza mapato zaidi.

Uwekezaji unaotokana na wanachama wa Zati hivi sasa ni dola 500 milioni za Marekani licha ya awali ulikuwa ukikabiliwa na matatizo ya vitega uchumi na kuchelewesha upanuzi wa sekta ya utalii nchini Zanzibar.

Kutokana na tatizo hilo shirikisho hilo lilifanya utafiti ambao ulifadhiliwa na BEST AC ili kukusanya mawazo ya kusaidia kutengenezwa kwa sheria ya kufuatilia mwenendo wa utalii na jinsi ya kukabiliana na uhalifu visiwani Zanzibar.

Kutokana na utafiti huo Zati imelenga kuishawishi Serikali kuboresha sheria zinazohusu uhalifu katika sekta hiyo. Sheria hiyo itasaidia kuundwa kwa mahakama maalumu ambayo itakuwa ikishughulikia matukio ya uhalifu wanayofanyiwa watalii visiwani humo.

Mwenyekiti wa Zati, Abdul Samad amesema ni muhimu kwa watalii kuwa na ulinzi wa uhakika ili kulinda sekta ya utalii, wadau na uwekezaji wake.

### Sekta ya utalii ilindwe

Ofisa wa Zati, Pamela Matthews anasema ipo haja kubwa kuilinda sekta ya utalii visiwani Zanzibar kwa kuwa ndio chanzo kikubwa cha mapato na kazi yenye heshima kwa Wazanzibari na Watanzania kwa ujumla.

Pamela anabainisha kwamba sekta hiyo inaajiri watu 15,000 wa kudumu na wengine 50,000 ambao siyo waajiriwa wa kudumu.

Anasema mfumo bora wa sheria utaboresha hali ya usalama na kuwashawishi watalii wengi kutembelea vivutio vya utalii Zanzibar.

"Kitendo cha kushindwa kuboresha ulinzi na usalama kutasababisha watalii kupungua Zanzibar, kupatikana kwa mapato kidogo na kuvuruga ajira zenye heshima visiwani huko," anabainisha Pamela.

Pamela anasema wadau ambao wako tayari kuzungumzia suala la ulinzi na usalama wanaweza kuwasiliana nao kupitia info@zati.org

Waziri wa Habari, Utalii na Utamaduni wa Zanzibar, Said Ali Mbarouk anasema Serikali inatambua umuhimu wa utalii na kwamba wizara yake ipo tayari kupokea maoni na jinsi ya kuboresha sekta hiyo.

"Serikali inasheria zinazopambanua masuala ya ulinzi na usalama kwa ujumla wake na hata katika sekta ya utalii, lakini kama Zati ikifuata kanuni za kawaida na kutuletea mapendekezo namna njema ya kuboresha ulinzi na usalama sisi tupo tayari kufanyia kazi maoni yao," anafafanua Mbarouk.

Anasema Serikali iko makini katika kuwalinda watalii kwa kuwapatia ulinzi na kwamba imeanzisha doria maalumu katika maeneo ya utalii ili kukabiliana na wahalifu.

Anaeleza kwamba lengo la kuwa na kikosi maalumu cha usalama ni kuhakikisha watalii hawabugudhiwi na wahalifu.

Kama ilivyo Tanzania Bara ambako uhalifu dhidi ya watalii umeripotiwa pia Zanzibari tatizo hilo ni tishio kwa watalii na katika ukuaji wa uchumi.

Pamela anabainisha kwamba tatizo la ulinzi na usalama linatosha kuzuia watalii kutembelea Zanzibar na kwamba mikakati ya kutosha inapaswa kuandaliwa ili kudhibiti uhalifu visiwani Zanzibar.

Mbarouk anasema wimbi kubwa la utalii visiwani Zanzibar linategemea zaidi jinsi serikali inavyowadhibiti wahalifu wanaotaka kuitia doa sekta hiyo.

### Watalii watapungua

Kitendo cha kushindwa kuhakikisha usalama kwa watalii kinaweza kuleta shida kubwa siku za baadaye hasa kwenye uchumi wa Zanzibar. Kama watalii watapungua Zanzibar kutasababisha kushuka kwa pato la taifa.

Kwa muongo mmoja sasa na zaidi, Zati imekuwa msemaji kwenye sekta binafsi na mara zote imekuwa ikiwataka wanachama wake watoe huduma bora za utalii, kuzingatia maadili, kufuata sheria za ushuru za Zanzibar, kufuata kanuni za fedha, mazingira, na kazi.

Pia Zaki imekuwa ikiwahimiza wanachama wake kununua bidhaa kutoka visiwani na kuajiri wananchi wa visiwani na pia miradi ya utalii inapaswa kuwashirikisha wananchi.

**Tujadiliane kupitia Ujumbe mfupi SMS kwa 15774 ukianza na neno BIZ na kufuatia ujumbe wako. Ujumbe wako mfupi ni bure, hautozwi.**

### DONDOO

**1. Utalii wa Zanzibar ni wa kipekee duniani ukilinganisha na mataifa mengine ya Afrika Mashariki ambao utalii wake mkubwa ni mbuga za wanyama.**

**2. Serikali ya Zanzibar inafikiria kuvifanya visiwa vya Unguja na Pemba kuwa kituo pekee cha kwanza kwa utalii ukanda wa Bahari ya Hindi ikitoa kwa kutoa huduma za hali ya juu za utalii katika miaka 17 ijayo.**

**3. Zanzibar inapanga kuendeleza utalii wake na kuufanya uwe wenye mvuto wa kipekee.**

BEST-AC
Tuboreshe mazingira ya biashara
Doing business, let's make it easy
UKURASA HUU UNADHAMINIWA NA BEST-AC NA MWANANCHI